BE READY.
STAY COVERED.

Maswali Yanayoulizwa Sana kuhusu Kujiandikisha Upya kwa Medicaid

Je, kujiandikisha upya kwa Medicaid ni nini?

Kila mwaka, Jimbo linapitia taarifa za washirika wa Medicaid kuhakikisha kuwa bado wanastahiki. Wakati mwingine hatua hii huitwa “kujiandikisha upya”. Ikiwa una taarifa za kutosha, tutakutumia notisi (Notisi ya Uamuzi kuhusu Fidia) ikikuambia kuwa tumeandikisha upya Medicaid yako.

Tukihitaji taarifa zaidi, tutakutumia notisi mbili:

- notisi ya manjano ya kujiandikisha upya kwa Medicaid
- notisi nyeupe ikikuomba nyaraka za ziada.

Notisi hizi mbili zitafika katika barua tofauti. Hakikisha kuwa umeziangalia zote mbili.

Je, ni wakati gani ninaopaswa kujiandikisha upya?

Si kila mtu atapata notisi yake katika barua kwa wakati sawa. Notisi hizi hutumwa kwa watu tofauti mwanzoni mwa kila mwezi. Unaweza kutumia Tovuti ya Medicaid Renewal Lookup kupata tarehe yako ya kujiandikisha upya kwa Medicaid. Tovuti ni rahisi na salama na huhitaji barua pepe wala nenosiri ili kuitumia. Tovuti inapatikana katika Kiingereza, lakini unaweza kuibadilisha hadi Kihispania au Kireno. Ikiwa mtu mwingine anakusaidia, anaweza kutumia tovuti pia.

Haya hapa mambo unayohitaji kufanya:

- Weka nambari ya kitmabulisho ya Medicaid kwenye kadi yako nyeupe ya Anchor.
- Weka tarehe ya kuzaliwa.

Tovuti itakuambia wakati unaweza kutarajia kujiandikisha upya. Lakini kumbuka, tarehe yako ya kujiandikisha upya inaweza kubadilika, hivyo angalia mara kwa mara.

Pia unaweza kupata tarehe ya kujiandikisha upya kwa Medicaid inayotarajiwa kwa kuingia kwenye akaunti yako katika healthyrhode.ri.gov na kutafuta “Taarifa Zangu za Kujiandikisha Upya.”

Nilipata notisi katika barua inayosema kuwa ninahitaji kutoa taarifa zaidi ili Jimbo lipitie ustahiki wangu. Je, ninaweza kuwasilisha vipi nyaraka zangu kwenye Jimbo?

Kuna njia nyingi unazoweza kutumia kuwasilisha taarifa kwenye Jimbo, ikiwa ni pamoja na mtandaoni, kwa barua, au ana kwa ana.

- **Programu ya mtandaoni au ya mkononi:** Tembelea healthyrhode.ri.gov ili ufikie akaunti yako mtandaoni au pakua programu ya mkononi ya HealthyRhode kwenye simu yako mahiri ili ufikie akaunti yako.
- **Kwa barua:** Unaweza kutuma nyaraka zako kwa P.O. Box 8709, Cranston, RI 02920-8787.
- **Ana kwa ana:** Mfanyakazi kwnye ofisi zae Rhode Island Department of Human Services (DHS, Idara ya Huduma za Binadamu) anaweza kuwasaidia wateja ana kwa ana. Kwa orodha ya ofisi za DHS na kuchanganua vituo, tembelea dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices.

Je, ninaweza kufanya nini ili kujitayarisha kwa ajili ya kujiandikisha upya?
Kuna mabo matatu unayoweza kufanya ili ujitayarishe na uendelee kuwa na bima.

1. **Sasisha taarifa za akaunti yako mara kwa mara** ili Jimbo liweze kuwasiliana nawe likiwa na taarifa muhimu. Kwa mfano, unapaswa kusasisha akaunti yako ikiwa taarifa zako za mawasiliano zimebadilika, umepata kazi mpya, au una mtoto.
2. **Angalia barua kutoka Jimbo la Rhode Island.** Ikiwa mpango wa Medicaid unahitaji taarifa zaidi ili kuandikisha upya bima yako, utapata notisi ya manjano. Pia utapata notisi nyeupe inayosema, "Nyaraka za Ziada Zinahitajika" (tutatuma notisi hii kando). Vinginevyo, utapata notisi inayosema kuwa bima yako imewezeshwa kuendelea kiotomatiki.
3. **Chukua hatua mara moja.** Ukipata notisi ya manjano, inamaanisha kuwa Jimbo linahitaji taarifa zaidi kukuhusu wewe au watu katika familia yako ili kuandikisha upya bima yako.

Je, ninaweza kusasisha taarifa zangu za mawasiliano?
Unaweza kusasisha taarifa zako za mawasiliano kwa njia kadhaa:

- **Mtandaoni au programu ya mkononi**: Tembelea healthyrhode.ri.gov ili ufikie akaunti yako mtandaoni au pakua programu ya mkononi ya HealthyRhode kwenye simu yako mahiri ili ufikie akaunti yako. HealthSource RI (HSRI) pia inatoa huduma za chati ya wavuti ya moja kwa moja wakati wa saa za kazi kwenye healthsourceri.com.
    - Washirika wote wa Medicaid wana akaunti iliyofunguliwa wakati uliidhinishwa kupata Medicaid. Ikiwa unafungua akaunti yako kwa mara ya kwanza, unaweza kuweka nambari ya ruzuku ya serikali na tarehe yako ya kuzaliwa ili upate jina la mtumiaji. Kisha fuata hatua ili ubadilishe nenosiri lako.
- **Wasiliana na shirika lako la huduma inayodhibitiwa na bima ya afya**: Je, una kadi ya bima kutoka Neighborhood Health Plan of Rhode Island, Tufts Health Plan (RITogether) au United Health Care Community Plan (UHCCP)? Piga simu nambari iliyo nyuma ya kadi yako kwa usaidizi wa kusasisha taarifa zako za mawasiliano.
- **Kwa simu**: Pigia simu HSRI kwa 1-855-840-4774 (Jumatatu hadi Ijumaa, isipokuwa sikukuu, kutoka saa 8 asubuhi hadi saa 6 jioni).
- **Ana kwa ana**: Mfanyakazi kwnye ofisi zae Rhode Island Department of Human Services (DHS, Idara ya Huduma za Binadamu) anaweza kuwasaidia wateja ana kwa ana. Kwa orodha ya ofisi za DHS, tembelea dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices.

Je, ninahitaji kufanya kitu chochote tofauti ili kuandikisha upya bima yangu na ya mtoto wangu?
Inawezekana kwa watu wanaoishi katika nyumba moja kupata aina tofauti za notisi za kujiandikisha upya. Kwa mfano, unaweza kupata notisi inayosema kwamba bima ya mtoto wako mtegemea ya Medicaid inaendelea kiotomatiki. Kutokana na hilo, huhitaji kufanya chochote kuandikisha upya bima yake. Huenda ukapata notisi ya pili kwa wakati mmoja inayosema kuwa wewe au wengine katika familia yako lazima watoe taarifa zaidi kwa Jimbo ili kuamua ustahiki. Ni muhimu uwasilishe nyaraka zilizoombwa kufikia makataa yaliyo kwenye notisi yako ya kujiandikisha upya.

Je, ninaweza kupata vipi usaidizi wa kujiandikisha kupya kwangu?
Usaidizi unapatikana ana kwa ana, kwa njia ya simu na mtandaoni. Ili kupata maelezo kuhusu machaguo haya, tembelea staycovered.ri.gov/medicaid-renewals/contact-us.

- Washauri wa Maombi na Waongozaji Waliothibitishwa wanapatikana ili kutoa usaidiziwa ana kwa ana bila malipo. Mashirika mengi ya jamii pia yanaweza kukusaidia kuelewa notisi yako ya kujiandikisha upya kwa Medicaid na hatua zinazofuata.
- Ikiwa una umri wa miaka 60 au zaidi au wewe ni mtu mzima aliye na ulemavu, unaweza kupigia simu Point, 401-462-4444. Ikiwa una umri wa miaka 65 au mpokeaji wa Medicare, unaweza kupiga simu, 888-884-8721. Washirika kwenye vituo vikuu na mashirika ya hatua za jamii yanaweza kusaidia pia.
- Ili kupata karibu na wewe, tembelea staycovered.ri.gov/community-support.

Nilikosa kutimiza makataa yaliyo kwenye kifurushi changu. Je, ninapaswa kufanya nini?
Ikiwa ulikosa kutimiza makataa yaliyo kwenye kifurushi chako cha manjano, tia sahihi fomu ya kujiandikisha upya na uwasilishe nyaraka zako mara moja.
Ikiwa Jimbo litapata kifurushi chako ndani ya siku 90 za tarehe ambayo manufaa yako yalisimama (kulingana na Notisi yako ya Uamuzi wa Manufaa), nyaraka zako zitakubaliwa na ustahiki wako utapitiwa.

- Ikiwa Jimbo litapata nyaraka zako ndani ya siku 90 na kuamua kuwa unastahiki Medicaid, bima yako itarejeshwa. Utapata Kadi ya Anchor unayoweza kutumia kwa matibabu na ziara za daktari ikiwa mtoa huduma atakubali ada ya huduma ya Medicaid. Kisha utaandikishwa upya ndani ya mpango wako huduma unaodhibitiwa (Neighborhood Health Plan of Rhode Island, Tufts Health (RITogether) Plan, au United Health Care Community Plan (UHCCP)).
- Jimbo likitapa nyaraka zako ndani ya siku 90 na kuamua kwamba hustahiki tena Medicaid, huenda ukapewa taarifa kuhusu jinsi ya kupata bima ya afya ya gharama ya chini kupitia HealthSource RI. Notisi yako ya Uamuzi wa Manufaa pia itakupa taarifa kuhusu jinsi ya kukata rufaa.

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu machaguo yako ya bima huku nyaraka zako zilizochelewa zikipitiwa, pigia simu HealthSource RI (HSRI) kutoka saa 8 asubuhi au saa 6 jioni siku za juma kwa 1-855-840-4774.

Je, nini kitakachotendeka nisipostahiki Medicaid?
Ikiwa hustahiki tena Medicaid, timu rafiki kwenye HealthSource RI inaweza kukusaidia kupata bima ya afya ya gharama ya chini.
Kutegemea na ukubwa wa familia na mapato yako, huenda ukastahiki:

- Kuandikisha kiotomatiki katika mpango wa afya unaostahiki (QHP) na usaidizi wa malipo ya bima wa miezi miwili
- Usaidizi wa malipo ya bima wa miezi miwili na vocha za kodi ya malipo ya bima ya serikali kuu
- Vocha za kodi za malipo ya bima za serijkali kuu husaidia kufanya bima ya afya kuwa nafuu zaidi.

Ukipata notisi inayosema kuwa hustahiki tena Medicaid lakini hukubaliani na uamuzi wa Jimbo, unaweza kuwasilisha rufaa.

Je, nini kitakachotendekea bima ya mtoo wangu nisipostahiki tena Medicaid?
Mtoto anaweza bado kustahiki bima ya Medicaid hata ikiwa mzazi wake au mlezi halisi hastahiki tena. Hii ni kwa sababu ustahiki wa mapato ya familia kwa watoto ni ya juu zaidi kuliko ya wazazi na watunzaji.

Ikiwa wewe na/au watoto wategemea katika familia yako hawastahiki tena Medicaid, timu rafiki kwenye HealthSource RI inaweza kukusaidia kupata bima ya afya ya bei nafuu.
Kutegemea na ukubwa wa familia na mapato yako, huenda ukastahiki:

- Kuandikisha kiotomatiki katika mpango wa afya unaostahiki (QHP) na usaidizi wa malipo ya bima wa miezi miwili
- Usaidizi wa malipo ya bima wa miezi miwili na vocha za kodi ya malipo ya bima ya serikali kuu
- Vocha za kodi za malipo ya bima za serijkali kuu husaidia kufanya bima ya afya kuwa nafuu zaidi

Je, mtoto "anatoka kiumri" kwenye Medicaid?
Wakati kijana wako anafikisha umri wa miaka 19 hastahiki tena Medicaid kuwa mtegemea katika familia ya Medicaid. Tunakagua vyanzo vyetu vya data ili kuona ikiwa tuna taarifa za kutosha za kuthibitisha ustahiki wa Medicaid wa umri wa miaka 19 katika kategoria nyingine (kwa kuwa si mtegemea wako tena). Tukithibitisha ustahiki katika kategoria nyingine, mtoto wa miaka 19 ataendelea kustahiki Medicaid kiotomatiki.

Wakati mwingine, hatuna taarifa za kutosha kuhusu mtoto wa miaka 19 au familia yako ili kuamua ustahiki. Hilo likitendeka, unapopokea notisi yako ya kujiandikisha upya kwa Medicaid, itasema "Hatua Inahitajika." Fuata maagizo yaliyo kwenye notisi yako ili uripoti mabadiliko katika hali ya familia yako. Pia utapata notisi nyeupe inayosema, "Nyaraka za Ziada Zinahitajika" (tutatuma notisi hii kando).

Hakikisha kuwa umetia sahihi notisi yako ya manjano ya kujiandikisha upya. Tafadhali tupe, pamoja na waraka wowote unaohitajika, **kabla ya tarehe ya mwisho** iliyo kwenye notisi yako ya manjano. Ni muhimu kurejesha nyaraka hizi ili tuweze kuamua ustahiki. Tusipopokea taarifa zako kufikia tarehe ya mwisho, bima ya Medicaid itasimamishwa. Ukikosa tarehe ya mwisho, una siku 90 kutoka tarehe ya mwisho kutuletea taarifa zako na ustahiki wako kurejeshwa.

Je, ninakata vipi rufaa?
Kuna njia chache za kuomba rufaa inayohusiana na bima yako ya Medicaid. Unaweza kukata rufaa:

- **Mtandaoni**. Ingia katika akaunti yako kwenye healthyrhode.ri.gov na ubofye "kata rufaa".
- **Kwa simu**. Unaweza kukata rufaa kwa kupigia simu HealthSource RI kwa 1-855-840-4774.
- **Ana kwa ana**. Kwa orodha ya ofisi za DHS, tembelea dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices. Fomu ya rufaa imejumuishwa katika kila Notisi ya Uamuzi wa Manufaa. Jaza fomu hii na uje nayo.
- **Kwa barua**. Fomu ya rufaa imejumuishwa katika kila Notisi ya Uamuzi wa Manufaa. Jaza fomu hii na uitume kwa ATTN: Appeals State of Rhode Island, P.O. Box 8709, Cranston, RI 02920-8787.

Maagizo kuhusu jinsi ya kukata rufaa pia yako katika Notisi yako ya Uamuzi wa Manufaa. Kwa maelezo zaidi, tembelea staycovered.ri.gov/medicaid-members/file-appeal.